# uhuru

*Basi Yesu akawaambia wale wayahudi waliomwamwini, ninyi mkikaa katika Neno langu mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli tena mtaifahamu kweli nayo kweli itawaweka huru. Wakamjibu, sisi tu uzazi wake Ibrahim, wala hatujawa watumwa wa mtu wakati wowote nawe wasemaje, Mtawekwa huru? Yesu aliwajibu amin amin nawaambia kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi wala mtumwa hakai nyumbani siku zote; mwana hukaa siku zote basi Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli. (Mt. Yohana 8:31-36)*

Hebu tusikilize kile Nabii wa Mungu wa kizazi hiki alichosema juu ya hayo.

Musa alikuwa anafahamu kwamba yeye atakuwa ndiye mkombozi kutokana na mafundisho ya mama yake na alijifundisha mambo ya vita vizuri ili kufanya hivyo lakini ilishindwa (kutoka 2:1-25) unaona? Alikuwa na ufahamu alikuwa na elimu, lakini hiyo haikusaidia kwa hiyo ilibidi asahau yote na aje kwenye kitu rahisi cha kumchukua Mungu kwenye Neno lake naye akawaokoa watu Ndiyo bwana. Mungu anaokoa kwa nini? Imani katika neno lake. Siku zote imekuwa hivyo……

Ninataka ninyi mkumbuke hili watu wa mataifa injili waliyopewa ni injili ya Imani siyo ya matendo hata kidogo unaona? Kama nilivyosema usiku wa jana. Roho Mtakatifu aliposhuka siku ya Pentecoste waliposhuka chini kule kwa wayahudi (matendo 19:1-6) ilibidi wawawekee mikono ili kumpokea huyo na walipoenda chini kule kwa wasamaria ilibidi waweke mikono yao juu yao lakini walipokuja kwa watu wa mataifa katika nyumba ya Kornelio wakati Petro alipokuwa akinena maneno hayo……..” hakuna kuwekewa mikono matendo 10:44-48)

Wakati yule msichana mdogo alipokuja binti yairo kuhani alisema “njoo umuwekee binti mikono naye ataishi” (Marko 5:21-23, 35-43)

Lakini yule akida wa kirumi mtu wa mataifa alisema “sistahili wewe uje chini ya dari yangu, nena Neno” (Matayo 8:5-13) hiyo hapo.

Mwanamke msirofoinike myunani hasa ndivyo alivyo.Yesu alimwambia, akisema “siyo vizuri kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa” mwanamke alisema “Naam Bwana lakini hata mbwa walio chini ya meza hula makombo ya watoto” akasema kwa sababu ya Neno hilo, pepo amemtoka binti yako (Marko 7:24-30, Matayo 15:21-28) Semeni basi maneno mazuri sema neno zuri juu ya mtu fulani zungumza juu ya Yesu sema kitu fulani cha uaminifu kitu halisi hiyo ndiyo namna



ya kutoa mapepo kamwe hakumuombea yule msichana hakusema chochote juu ya uponyaji wake Alisema tu “Kwa neno hili, kwa neno hili…..”

Hattie wright siku ile hukuomba kitu chochote alikuwa ameketi tu pale lakini alisema kitu sahihi kilichompendeza Roho Mtakatifu naye Roho Mtakatifu alizungumza na kasema “Hattie omba chochote utakacho chochote ulichonacho na unachohitaji Tafuteni muone kama hilo ni halisi au sio omba chochote uponyaji wa dada yake mdogo aliyekiwete akiwa ameketi pale na miguu imesinyaa ndani, ikiwa ni dola elfu kumi ili asiendelee kulima kule milimani ujana wake urudishwe kwenye mwili wake uliomzee; chochote utakacho omba kiombe sasa hivi kama hakitakuja nami nikakupa hicho sasa basi mimi ni nabii wa uongo hicho ni kitu fulani si hivyo? (Naye aliomba wokovu wa watoto wake wawili na Roho Mtakatifu akampa hilo mara moja)

Usiku mmoja Mungu alipokusudia kwamba mwana kondoo lazima auwawe ikiwa ni mfano wa kristo na damu ikawekwa katika hissopo ambayo ni majani (manyenyekevu, yakawaida) na kuwekwa kwenye mwimo wa mlango na katika nguzo na hapo ndipo Israeli walipokuwa wamekombolewa kikamilifu, bila kuacha ukwato nyuma,vyote vilivyo vya kwao vilikombolewa familia zao, wapendwa wao, na kila kimoja kilikombolewa wakati walipokamilika kuja chini ya damu (kutoka 12:1-42)

Hapo ndipo kanisa litakapokuwa limekombolewa kikamilifu wakati kila kitu kitakapokuja chini ya damu dhambi zako zinapokuja chini ya damu, kuvuta kwako, kupiga kwako kamari, uongo wako, kuiba kwako, kudanganya kwako, wakati kila kitu kinapoletwa chini ya damu, hapo kutakuwa na ukombozi mkamilifu. Kama umemkosea mtu fulani, lisahihishe. Huwezi ukalileta hilo chini ya damu, halitakaa. Huwezi ukalileta, kitu fulani hakitaruhusu kufanya hivyo. Wakati wewe mwenyewe kwa ukamilifu, kwa ujumla umeletwa chini ya damu, kutakuwa na ukombozi mkamilifu. Hapo sasa utakuwa na uhuru ambao hujawahi kuufahamu kabla, wakati kila kitu kimeletwa chini ya damu, umeletwa na kuwa aliyejitolea kabisa kwa ufalme wa Mungu. Hapo sasa kutakuwa na ukombozi halisi.

Yesu alikuwa mkamilifu, mwanadamu hasa. Aliweza kulia kama mwanadamu, alikuwa anakula kama mwanadamu, aliweza kuwa kama mwanadamu. Alikuwa mkamilifu, mwanadamu hasa katika utu wake wa kimwili. Na katika Roho yake, Alikuwa mkamilifu, Mungu hasa, kwa hiyo aliufanya mwili wake uwe mtiifu kwa Roho iliyokuwa ndani yake. Unaona, alijaribiwa katika njia zote kama sisi alikuwa mwanadamu sio malaika, alikuwa mwanadamu. Alikuwa na shauku na majaribu kama tulivyo (Waebrania 4:14 – 16). Biblia ilisema hivyo. Alikuwa mwanadamu, siyo Malaika aliye juu ya majaribu Waebrania 1:4 ilisema. Alifanyika mdogo kuliko Malaika (Waebrania 2:5 – 10). Alikuwa mwanadamu, mwanadamu mkamilifu, kwamba Mungu alichukuwa mwanadamu mkamilifu kuleta ukombozi mkamilifu, na akamjaza yeye na Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu alikuwa ndani yake bila kipimo. Na alijaribiwa kama sisi. Na alikuwa ni Mungu mkamilifu (Yohana 1:1 – 3, 14 – 18, Kolosai 1:14 – 15, 1Yohana 5:20). Alithibitisha hilo alipofufuka kutoka kwa wafu,

aliposimamisha maumbile, bahari iliyonguruma na pepo zenye nguvu. Alipozungumza na miti, na kadhalika, ilimtii, Yeye. Ndani alikuwa Mungu (2Kor5:18 – 19, Waebr.1:1 – 3). Na aliweza kuwa mwanadamu, kwa kuwa alikuwa mwanadamu, lakini kijumla na alijitolea kikamilifu yeye mwenyewe na kujiweka mkononi mwa Mungu kwa ajili ya huduma ya Mungu. Na ni mfano wetu.

Sisi tu wanaume na wanawake. Na pia tu wakristo kama yeye ni mfano wetu, natujitolee kikamilifu mkononi mwa Roho Mtakatifu, ilituwe washirika wa ufalme wa Mungu.

Alikuwa mwanadamu hasa, alikuwa ni Mungu hasa, lakini alisalimisha sehemu yake ya maumbile na sehemu yake inayoonekana na mawazo yake mwenyewe, na utendaji wake na mambo yake mwenyewe, na "Ninafanya tu yale yanayompendeza Baba" (Yohana 5:19) Unaona hilo. Kukombolewa hasa kutoka katika utu wa kibinadamu.

Na wakati mtu anaposema analiamini Neno, na halafu Roho Mtakatifu anapokuja, ni hati ya umilikaji. Na hiyo inakupa ruhusa, unapokuwa wewe ni mmilikaji, kwamba kila kitu cha hiyo ni mali yako, na kila kitu katika hiyo ni mali yako. Amen.

Na hiyo inatupa sisi umiliki, wakati Roho Mtakatifu anapokuja juu ya hii hati miliki kwamba Mungu alituona nyuma kule kabla ya kuwekwa misingi ya dunia na akaweka Jina katika kitabu cha uzima, lakini alizaliwa kupitia mwanaume na mwanamke, na awezaye kukosa, na kuwa na hatia ya dhambi. Lakini nilipoamini katika hilo, nilipokea hati.

Lakini wakati Roho Mtakatifu alipokuja alikuwa ni uhakika kwamba kila kitu kinyume na mimi, ikiwa ni mama alikifanya, baba yangu alikifanya, bibi yangu alikifanya (kama yule mtoto mdogo aliyekuwa na kifafa niliyemuombea dakika chache zilizopita, hicho kimekuja kutoka kwa mababu …….. hicho kifafa kikaja chini na …….juu ya mtoto, nikasema), lakini ule uhakika unapokuja, inafutilia mbali na kuondoa kila kitu. Mimi ni anayeshikilia hati miliki ya uhakika sasa. Amin. Na kwa uhakika wa Roho aliye mfufua Kristo kutoka kwa wafu, ninayo hati miliki hakika kwamba mimi ni sehemu ya ule mwili, pamoja na uthibitisho wa Roho Mtakatifu aliyeufanya huo mwili wa Neno uishi vile hasa ulivyofanya ndani yake kama alivyo ahidi katika siku za mwisho, ule uhakika.

Dhambi zangu zote zimeondolewa. Dhambi zako zote zimeondolewa kwa damu ya Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu amekuja na uhakika wa hati miliki kwamba Mungu amenipa mimi kwa Neema na ufahamu wake wa kimbele Oh jamani.

Nini unaogopa? Siajabu alisema, "usiogope, mimi nilikuwa nimekufa na sasa ni hai tena, na ni hai milele na milele na ninazo funguo za mauti na kuzimu. Usiogope juu ya chochote, hata mauti haitakudhuru wewe" (Ufunuo 1:18).



Angalia, nzuri sana. Hebu twende kwa haraka sasa. Ule uhakika wa umiliki. Deni imelipwa, kila kitu kinyume na hiyo kimefutwa. Ha, ha, ha, utukufu.

Ninaweza nikatenda kama mjinga , lakini najisikia vizuri, angalia. Unaona? Oh uhakika wa hati unafahamu hiyo inamaanisha nini? Unafahamu hiyo inavyomaanisha, Ndugu hakuna kitu kinachoweza kuiondoa kwako, Amini. Mimi ni mmiliki. Amin.

Hati ya namna gani? Sasa hivi gharama/fedha imelipwa katika faida yangu ya kufa kwake, kuzikwa, na kufufuka amekuwa mimi kwamba niwe Yeye sasa alikuwa mdhambi ili niwe mwana (Amini) na nishikilie uhakika wa hati kwa "Ishara hizi zitafuatana nao waaminio", hati miliki.

Unaona, Bibi Arusi wa mataifa yuko mbinguni (wakati wa miaka 31/2 ya dhiki kuu) na mwanamwali mpumbavu, mwanamwali wa mataifa hataokolewa wakati huo, yeye ameshaokolewa tayari lakini amekataliwa katika Bibi Arusi na anaenda tu kupitia dhiki kuu kwa wakati wa utakaso kwa sababu amemkataa Kristo Neno kwa ajili ya utakaso wake. Kwa hiyo inabidi ateseke kwa ajili ya tendo lake hilo lakini Bibi Arusi ambaye amekuwa Neno upatanisho mkamilifu kwa Kristo (1Yohana 2:2) kwa sababu yeye ni Neno ule mwili ulipotolewa na ule mwili ulipotolewa Bibi Arusi alikuwa ndani ya ule mwili kwa sababu ni Neno lote Amini unaona hilo?

Yesu alipoteseka katika mwili aliteseka….. kwa sababu mwanaume na mwanamke ni mtu mmoja. Hawa alitolewa kutoka kwa Adamu na kanisa …….kumetokea nini? Mungu alifungua ubavu wa Adamu na akachukuwa kutoka hapo msaidizi, Bibi Arusi na Mungu alifungua ubavu wa Yesu pale msalabani na kuchukua bibi Arusi (Waefeso 5:30-32, Mwanzo 2:21-25) unaona? Na Yesu alipokufa pale msalabani kumbuka Bibi Arusi alikuwa hajachukuliwa kutoka kwenye mwili mpaka ule mwili ulipokufa. Alikuwa tayari amekufa, na walikuwa wanaenda kumvunja miguu yake. Na nabii alisema, "Hakutakuwa na mfupa wake utakaovunjwa" (Yohana 19:31-37, Zaburi 34:20) kwa hiyo waliinua nyundo tayari kumvunja mguu na mtu akakimbia na upanga na kuusukumia ndani moyoni na maji na Damu vilitoka Alikuwa tayari ameshakufa alikuwa tayari amekombolewa katika mwili kwa kufa kwake kwa hiyo hakuna kuteseka kipindi cha dhiki kwa Bibi Arusi unaona? Anaenda ndani lakini Kanisa la mataifa wale wanaoamini tu kwake na kuchukua kanuni za kidhehebu nakadhalika…….

Ndugu Brahamu aliulizwa je itakuwaje kwa watu wanao mwamini Bwanasasa na sio katika njia unayohubiri?

Hawapaswi kuamini hili. Sio lazima waamini kwa njia ninayohubiri unaona? "Hawapaswi kuamini hilo…." Ujumbe wa wakati wa mwisho. "Je wataokolewa?" Ndiyo kama wanamuamini Bwana. Unaona? Na kama hawakubaliani na kusema, "Siamini yeye ni Neno. Siamini kwamba hii ni kweli. Siamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu", hiyo inaonyesha wanaenda wapi, kwenye dhiki kuu. Lakini wale wanaoweza kuamani Neno katika ukamilifu wake, sio mimi ninalihubiri, ni kwa

sababu ni Biblia inasema hivyo. Wale wanaokubali wako huru, kwasababu Neno tayari limekwisha hukumiwa (Yohana 5:24).

**<u>Nukuu za kiingereza</u>**
"Mungu katika Urahisi" (63 – 0317M), Kitabu cha mihuri Uk. 30, Aya 175/ "Maswali na majibu juu ya Roho Mtakatifu", Aya 17 – 21/ "Ukombozi mkamilifu", Aya 85 – 89/ "Ni kule kuchomoza kwa jua", uk. 36/ "Maswali na majibu" (64 – 0823M), COD uk 953 – 955, Aya 151 – 152 – 157.

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 119 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69, D-75328 schomberge, Germany, Simu (+49) 72357613 Fax +(49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundihso uk. 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*